HOTUBA YA KAMISHNA WA MAADILI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA TAREHE 22-23 OCTOBA, 2026 KATIKA UKUMBI WA HOTELI YA ROYAL TUGHIMBE -MBEYA

Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

Mwakilishi wa TUGHE Taifa;

Mwakilishi wa TUGHE Mkoa;

Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

Waandishi wa Habari;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndugu Wajumbe,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuwawezesha kusafiri salama kutoka maeneo mbalimbali ambako ni vituo vyenu vya kazi hadi hapa Mbeya kwa ajili ya kushiriki Mkutano huu muhimu kwa Taasisi yetu ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Vilevile, niwashukuru nyote na wenzenu mnaowawakilisha katika kikao hiki kwa ushirikiano mnaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi tuliyokabidhiwa; asanteni sana na karibuni katika mkutano huu.

Ndugu Wajumbe;

Tukiwa tunaendelea na utekelezaji wa Waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 1970 ambao unaelekeza kila Taasisi ya Umma kuwa na Baraza la Wafanyakazi, tunakutana tena katika Mkutano huu ili tuweze kujadiliana kuhusu utekelezaji wa majukumu yetu na mipango yetu ya bajeti.

Katika Mkutano wetu wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika tarehe 18 Machi, 2026 tuliongea na kujadiliana kuhusu mipango ya bajeti kabla ya kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika mkutano huu wa siku mbili tutapokea taarifa ya mikakati mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti yetu kwa mwaka wa 2026/2027, kwa ajili ya kujipanga vizuri namna ya kutekelezaji majukumu tuliyodhaminiwa kwayo kwa uafanisi zaidi.

Hivyo basi, ninaomba kutumia fursa hii kuomba ushiriki wenu wa hali ya juu katika mkutano huu ili tuweze kufanikisha malengo yetu.

Naomba niwakaribishe kwa mara nyingine, KARIBUNI SANA.

Ndugu Wajumbe;

Napenda kuweka wazi kuwa Ofisi yetu inaendelea na jitihada za kuhakikisha changamoto zinazotukabili zinapungua kwa kiasi kikubwa ili majukumu yetu yasikwame. Hatua hizo ni kama zifuatazo

Kuhusu majengo ya ofisi, kwa upande wa Kanda ya Ziwa, changamoto kadhaa zilikuwepo na ambazo

zimepatiwa ufumbuzi na kwa sasa ujenzi unaendelea. Kwa upande wa mradi wa ujenzi Kanda ya Mashariki na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

Vilevile, kwa kutambua uhaba uliopo wa magari, Ofisi imetenga kiasi cha fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari likiwepo basi aina ya coaster kwa ajili ya watumishi. Mchakato wa ununuzi wa magari hayo uko katika hatua za mwisho na magari hayo yatagawanywa kulingana na kipaumbele cha mahitaji.

Ndugu Wajumbe;

Ninayo furaha kuwajulisha kuwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 Taasisi ilipewa nafasi thelathini na nne (34) na kati ya nafasi hizo tayari watumishi ishirini na saba 27 wameripoti vituo vya kazi na kupangiwa kazi na pia wote wamepatiwa mafunzo ya awali (induction course)

Kwa sasa Taasisi ina watumishi **234** kati yao **226** ni waajiriwa wa Taasisi na watumishi 8 wameazimwa kutoka Taasisi nyingine. Napenda pia kuwajulisha kuwa Muundo wa Taasisi uliohuishwa, na kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania Mh. Dkt Samia Suluhu Hassan kuanzia tarehe 9/7/2025, kwa sasa zoezi la kujaza nafasi mpya zilizobainishwa linaendelea.

Ndugu Wajumbe;

Katika kuendelea kutekeleza majukumu yetu tuliyokabidhiwa ni vema tutambue kuwa tumepewa dhamana ya kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake, na sisi ndiyo taswira ya Taifa letu linapokuja suala la uadilifu. Rai yangu kwenu ni kuendelea kutekeleza majukumu mliyonayo kwa weledi na uadilifu wa kiwango cha juu na kwa Maslahi mapana ya Taifa letu.

Ndugu Wajumbe,

Aidha, ili kufanikisha malengo ya Taasisi yetu, suala la ushirikiano baina yetu halina mbadala hivyo ninawaomba ushiriki wa kila mmoja katika kufanikisha malengo ya Taasisi. Kila mtumishi kwa nafasi yake na kwa ushirikiano, atekeleze majukumu kwa weledi, maarifa, jitihada na mapenzi akitambua kuwa anategemewa kwa nafasi aliyonayo na kwamba yeye ni kipande katika mkufu.

Ninaomba sote tufahamu kuwa katika utekelezaji wa majukumu yetu tunapokea maelekezo kutoka maeneo tofauti ambayo tunapaswa kuyatekeleza kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na weledi. Kwa kuwa tumeajiriwa ili tufanye kazi hivyo tuache uzembe, uvivu na mazoea katika kutekeleza majukumu yetu. Tusiwe chanzo au sababu ya kuikwamisha Serikali kutekeleza majukumu yake.

Ndugu Wajumbe;

Kwa kuwa tutapata fursa ya pamoja na mambo mengine kujadili kuhusu utekelezaji wa bajeti ni matarajio yangu kuwa wote tutakuwa na uelewa wa pamoja kuhusiana na vipaumbele vya Taasisi katika mwaka husika na kwamba kila mmoja kwa nafasi yake atatimiza majukumu yake ipasavyo ili kuwezesha Taasisi kufikia malengo yake

Ndugu Wajumbe;

Ninapenda kuwashukuru kwa mara nyingine tena kwa kuhudhuria kwenu katika Mkutano huu wa Baraza. Naamini yote yatakayowasilishwa na ambayo yatahitaji utekelezaji wenu mtayafanyia kazi kwa wakati. Kwa mara nyigine napenda kuwakumbusha watumishi wote wa Sekretarieti ya

Maadili ya Viongozi wa Umma kufanya kazi kwa bidii, kuwa wabunifu,waadilifu, wenye kujituma, kushirikiana na kuhakikisha tunatunza siri za Serikali.

Baada ya maelezo hayo, ninatamka kuwa Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi **UMEFUNGULIWA RASMI.**

ASANTE SANA KWA KUNISIKILIZA